# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS

Telegrams: "UTUMISHI", DAR ES SALAAM
Simu : +(255) 22 2118531-4
Fax No.: +(255) 22 2125299
E-mail: permsec@utumishi.go.tz

Utumishi na Utawala Bora,
Jengo la Utumishi,
8 Barabara ya Kivukoni,
S.L.P 2348,
11404 DAR ES SALAAM.

*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb. Na.** CDC.228/297/01/6

30 Mei, 2016

## WARAKA WA UTUMISHI NA. 1 WA MWAKA 2016 KUHUSU UTARATIBU WA KUSHUGHULIKIA KIMKAKATI AJIRA ZA WATAALAM WA KITANZANIA KATIKA TAASISI ZA KIMATAIFA NA KIKANDA

### 1.0 Utangulizi

1.1 Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama wa Taasisi mbalimbali za Kimataifa na Kikanda. Faida zinazopatikana kutokana na nchi yetu kuwa mwanachama ni pamoja na kupata fursa mbalimbali zikiwemo ajira za Wataalam wa Kitanzania katika Taasisi hizo. Ajira hizi hutoa fursa kwa Wataalam hao kuongeza upeo, ujuzi na uzoefu katika nyanja mbalimbali. Uzoefu wanaoupata wataalam hawa hutumika kuongeza tija na ufanisi katika utendaji kazi Serikalini pindi wanaporejea nchini baada ya kumaliza mikataba yao. Aidha, kuwepo kwa watanzania kwenye Taasisi hizi hususan katika nafasi muhimu kunasaidia kutetea masilahi ya nchi katika nyanja mbalimbali za maendeleo. Vile vile mishahara na marupurupu mengine wanayolipwa huko huchangia katika kukuza pato la Taifa.

1.2 Katika kuhakikisha kuwa fursa za ajira za Wataalam wa Kitanzania katika Taasisi za Kimataifa na Kikanda zinatumiwa vizuri kwa manufaa ya Taifa, Serikali ilitoa Waraka wa Utumishi Na. 9 wa mwaka 1992 uliohusu Utaratibu wa Kuajiri na Kutumia Vizuri Wataalam Wazalendo Nje na Ndani ya Utumishi wa Umma. Vile vile zimekuwapo jitihada za kufuatilia fursa za ajira zinazopatikana katika Taasisi za Kimataifa na Kikanda; kutoa taarifa za nafasi za kazi zilizojitokeza; kuwahimiza Wataalam wa Kitanzania kujitokeza kuomba nafasi hizo; na inapowezekana, kutoa mafunzo kuhusu usaili kwa waombaji wa kazi kwenye nafasi hizo.

## 2.0 Changamoto

Pamoja na jitihada hizi, bado idadi ya Wataalam wa Kitanzania wanaoajiriwa au kushika nafasi muhimu za uongozi na za kitaalam ***(Strategic and Professional Positions)*** kwenye Taasisi hizi ni ndogo. Hali hii imesababishwa na changamoto zifuatazo:-

2.1 Baadhi ya Watanzania kutokujua utaratibu unaotakiwa kufuatwa katika kuomba ajira hizi;

2.2 Baadhi ya Watanzania kutokuwa na moyo wa kuthubutu na kujiamini kuomba nafasi hizo;

2.3 Taarifa za nafasi za kazi katika Taasisi za Kimataifa na Kikanda kupitia balozi zetu kutofika kwa wakati;

2.4 Baadhi ya Watanzania kutokutembelea tovuti mbalimbali, zikiwemo za Taasisi za Kimataifa na Kikanda au za kijamii ambazo hutangaza fursa za ajira katika Taasisi mbalimbali za aina hiyo;

2.5 Baadhi ya waajiri kutowaruhusu watumishi wao wanaopata nafasi za kazi katika Taasisi husika na kutowapokea pale wanapotaka kurudi katika ajira zao kutoka katika Taasisi hizo; na

2.6 Kukosekana kwa taarifa za kutosha zinazoonyesha idadi ya Wataalam wa Kitanzania wanaofanya kazi kwenye Taasisi za Kimataifa na Kikanda nje ya nchi. Taarifa hizi zingeliwezesha Taifa kupanga mikakati ya kuwatumia wanapokuwa katika nafasi hizo na baada ya ajira zao katika Taasisi hizo kukoma.

## 3.0 Madhumuni ya Waraka

Madhumuni ya Waraka huu ni kufafanua kuhusu utaratibu unaotakiwa kufuatwa katika kuomba ajira hizi na kuweka mkakati utakaowawezesha watanzania wengi wenye sifa kupata nafasi za kazi katika Taasisi za Kimataifa na Kikanda.

## 4.0 Utaratibu Unaotakiwa Kufuatwa katika Kuomba Nafasi za Kazi Katika Taasisi za Kimataifa na Kikanda

4.1 Watanzania wenye sifa zinazostahili, wataomba nafasi hizi moja kwa moja kwa kupitisha maombi yao kwa waajiri wao kwa kuzingatia masharti yaliyotolewa kwenye matangazo. Kwa nafasi zinazotakiwa kuungwa mkono na Serikali, Watumishi watapitisha maombi yao kwa waajiri wao na kuyawasilisha Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma (OR-MUU).

4.2 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma (OR-MUU) itayachambua maombi yaliyopokelewa na kutengeneza orodha fupi ya waombaji wenye sifa na kuwasilisha Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa kwa ajili ya kuwasilisha kwenye Taasisi husika.

4.3 Waombaji watakaofanikiwa kuitwa kwenye usaili watajulishwa na Taasisi husika au Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma (OR-MUU) kama itakavyoonekana inafaa.

## 5.0 Mambo ya Kuzingatiwa na Waombaji Watakaofanikiwa Kupata Nafasi za Ajira katika Taasisi za Kimataifa na Kikanda

5.1 Wataalam wa Kitanzania watakaofanikiwa kupata nafasi za ajira katika Taasisi za Kimataifa na Kikanda watatakiwa kuwasilisha kupitia kwa waajiri wao maombi ya kibali cha likizo bila malipo/kushikizwa OR-MUU kwa kipindi cha mkataba wa ajira.

5.2 Endapo Wataalam wa Kitanzania watatakiwa kuongezewa mkataba baada ya mkataba wa awali kuisha, watapaswa kuomba kibali cha kuongezewa muda kwa wakati Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma (OR-MUU).

5.3 Wataalam wa Kitanzania watakapokuwa wanakaribia kumaliza mikataba yao katika Taasisi za Kimataifa na Kikanda wakiwa na uhakika kuwa hawataongezewa mkataba, watatakiwa kutoa taarifa kwa waajiri wao kuomba kurudi kazini mwaka mmoja kabla ya mkataba kuisha ili mwajiri aweze kuandaa utaratibu wa kuwapokea kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo.

5.4 Aidha, kwa Wataalam ambao hawatapenda kurudi tena katika Utumishi wa Umma baada ya kumaliza mikataba yao watapaswa kutoa taarifa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma (OR-MUU).

5.5 Baada ya kurudi katika Utumishi wa Umma, Watalaam wa Kitanzania waliokuwa wakifanya kazi katika Taasisi za Kimataifa na Kikanda watapaswa kuwasilisha taarifa ya kazi walizokuwa wakizifanya kwa waajiri wao ili kuwawezesha waajiri kuwapangia kazi kutokana na uzoefu walioupata.

## 6.0 Mambo ya Kuzingatiwa na Waajiri

6.1 Waajiri wahakikishe kuwa maombi ya ajira za Wataalam wa Kitanzania katika Taasisi za Kimataifa na Kikanda yanapitishwa haraka na kuwasilishwa kwa mujibu wa maelekezo ya tangazo la kazi. Aidha kwa yale yanayotakiwa kuungwa mkono na Serikali yatapaswa kupitishwa na kuwasilishwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma (OR-MUU).

6.2 Kwa wataalam ambao watafanikiwa kupata ajira katika Taasisi hizo, waajiri watatakiwa kuwasilisha maombi ya likizo bila malipo kwa wakati katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma (OR-MUU) ili vibali vya kuwaruhusu kwenda kufanya kazi katika Taasisi hizo vitolewe kwa wakati.

6.3 Waajiri watakapopokea taarifa ya watumishi kurejea kazini kutoka katika Taasisi za Kimataifa na Kikanda, watatakiwa waweke utaratibu wa kuwapokea na kuwapangia kazi zinazokidhi utaalam na uzoefu walioupata ili kuongeza ufanisi, kulingana na Sheria, Kanuni na Taratibu.

## 7.0 Mikakati ya Kuwawezesha Watanzania Wengi Kupata Nafasi Katika Taasisi za Kimataifa na Kikanda

7.1 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma (OR-MUU) kupitia Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa itafuatilia kupata taarifa ya nafasi zitakazokuwa wazi katika Taasisi za Kimataifa na Kikanda mapema iwezekanavyo ili ziweze kutangazwa kwa wakati.

7.2 Kila mwajiri anatakiwa kuhakikisha kuwa anawahamasisha na kuwasisitiza wataalam wenye sifa zinazotakiwa kuomba

nafasi zilizo wazi katika Taasisi za Kimataifa na Kikanda kila zinapotangazwa.

7.3 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma (OR-MUU) itaainisha na Kutengeneza kanzidata (Database) ya Wataalam wa Kitanzania wenye sifa za kuomba kazi katika Taasisi za Kimataifa na Kikanda. Kanzidata hii itatumika kuwatambua kwa urahisi wataalam wa Kitanzania wenye sifa za kuomba nafasi hizi ili waweze kuomba pale zitakapojitokeza.

7.4 Kwakuwa baadhi ya lugha za kigeni zinafundishwa katika ngazi mbalimbali mashuleni, na kwakuwa tayari wapo watanzania wenye ufahamu wa lugha hizo, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma (OR-MUU) itaweka utaratibu wa kuwatambua na kuwahamasisha kuomba nafasi zitakazokuwa na masharti ya ufahamu wa lugha zaidi ya Kiingereza. Aidha, itawahamasisha watanzania wanaopenda kufanya kazi katika Taasisi za Kimataifa na Kikanda kujifunza lugha zaidi ya Kiingereza ili kuongeza soko lao la ajira.

7.5 Wataalam wa Kitanzania watakaoitwa kwenye usaili watapatiwa maelekezo kuhusu masuala ya kuzingatiwa wakati wa usaili. Utaratibu huu utawajengea ari ya kujiamini katika kushindania nafasi hizi.

7.6 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma (OR-MUU) kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa itaandaa taarifa za Wataalam wa Kitanzania wanaofanya kazi katika Taasisi za Kimataifa na Kikanda. Taarifa hizi zitaisaidia Serikali kuwatambua wataalam hao na kuona namna ya kuwatumia wanapokuwa huko na watakaporudi nchini.

## 8.0 Mwisho

8.1 Waraka huu utasomwa kwa pamoja na Waraka wa Utumishi Na. 9 wa Mwaka 1992.

8.2 Waraka huu utaanza kutumika tarehe 1 Julai, 2016.

Dkt. Laurean J. Ndumbaro
**KATIBU MKUU (UTUMISHI)**